

## TANGAZO/TANGAZO / TANGAZO

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Mh. Happyness William Seneda anawatangazia wananchi na wadau wote wa Maendeleo kuwa, Wilaya ya Kisarawe inatarajia kufanya Tamasha kubwa la "**Zaramo Festival**" siku ya **Jumamosi** tarehe **23/09/2017** katika viwanja vya shule ya Msingi Chanzige, Kata ya Kisarawe kuanzia saa 2:00 Asubuhi.

Lengo kuu la Tamasha hilo ni kuwaunganisha wakazi wa Wilaya ya Kisarawe kutoka ndani na nje ya Kisarawe na kupata fursa ya kuenzi na kujifunza utamaduni wa Kizaramo, kuona maonyesho ya ngoma mbalimbali za asili, sanaa za ufinyanzi, ususi, uchongaji, mapishi ya vyakula vya asili, vivutio vya utalii na uwekezaji na maonyesho ya bidhaa mbalimbali, za wajasiriamali wanaozalisha kutoka kwenye viwanda vidogo vidogo na vya kati

Wananchi wote mnakaribishwa Wilaya ya Kisarawe kuhudhuria na kushiriki katika Tamasha hili.